**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**MEI, 2025**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO**

**SHULE YA SEKONDARI NGERENGERE**

Namba za simu

Mkuu wa shule 0715-106414/0787-106414

Makamu mkuu wa shule 0677-724954/0759-357458

**Shule ya sekondari Ngerengere**

**S.L.P 23, Ngerengere**

**Tarehe 23 April 2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**…………………………………………………………………

S.L.P…………………………………………………………..

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NGERENGERE ILIYOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO, MKOA WA MOROGORO, MWAKA 2025/2026**.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2025/2026 na atasoma tahasusi ya……………….
   Shule ya Sekondari Ngerengere ipo umbali wa kilometa 78 kutokea morogoro mjini na usafiri ni wa basi au treni ya mwendokasi (SGR). Usafiri kutoka morogoro mjini upo mabasi ya kampuni ya SALMEEN BUS, MBWACHA BUS na MVULA BUS kuanzia saa 5 mpaka saa 9 alasili. Unapatikana katika kituo cha Mabasi Msamvu, nauli ni shilingi 7,000/=. Kwa wanaotoka mikoani kutumia barabara ya Morogoro-Dar es Salaam, shuka kituo kinachoitwa UBENA ZOMOZI na hapo utapanda magari madogo (tax) kuja NGERENGERE na gharama yake ni Tshs 3,000/= umbali wa kilometa 18. Ukifika Ngerengere stendi panda pikipiki waambie unaenda kwenye shule ya A'level Ngerengere na nauli ni Tsh. 1000/=. Kwa usafiri wa SGR ni kwa wale wanaotokea mikoa ya Dodoma,Morogoro na Dar es Salaam na mikoa ya jirani na hiyo ashuke station ya NGERENGERE.
   Mhula wa masomo unaanza tarehe 08/07/2025 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 06/07/2025.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

i. Sare ya shule ni suruali rangi ya ugoro (Brown). Iwe na marinda mawili mbele, pindo la chini ligeukie juu (turn up) isiyobana (modo) ndefu mpaka kwenye vifundo vya miguu . Mwanafunzi anatakiwa awe na jozi mbili za suruali.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi. Aina ya kitambaa ni tomato
iii. Sare ya michezo ni truck suit rangi ya bluu iliyokolea,bukuta ya bluu na T-shirt yha bluu isiyo na maandishi na raba (jozi moja )
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya **kufunga na Kamba** vyenye visigino vifupi.
v. Soksi jozi mbili nyeusi
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali
vii. Sweta moja rangi ya ugoro (Brown) shingo iwe ni ya V,pia liwe na mikono mirefu [masweta yatapatikana shuleni kwa shilingi 18,000/=]
viii. Nguo za kushindia ni T-shirt moja yenye nembo ya shule ambayo itapatikana shuleni kwa shilingi 15,000/= na suruali moja ya kitambaa rangi nyeusi, isiwe modo.
ix. Tisheti (T-shirt) maalumu kwa ajiri ya darasani rangi yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 15,000/=

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni**

i. Madaftari 7 (counter books) quire 4
ii. Ream (A4) ya karatasi za photocopy Bunda mbili (2) kwa mwaka
iii. Vitabu vya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)

VITABU VYA KIADA NA ZIADA

| ADVANCED MATHEMATICS | GEOGRAPHY | ECONOMICS | HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI |
|---|---|---|---|
| 1. Advanced mathematics for form 5 by TIE<br>2. PURE 1 Mathematics by Backhouse<br>3. Conceptual advanced mathematics for secondary | 1. Practical Geography for advanced secondary schools 5&6 by TIE<br>2. Physical Geography for advanced secondary schools | 1. Micro economics for advanced secondary schools form five by TIE<br>2. Micro economics Advanced secondary schools | Historia ya Tanzania na Maadili kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano (TIE) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| schools form five by Petro Mayombya | form 5&6 by TIE<br>3. Human Geography for advanced secondary schools f5&6 by TIE | form six by TIE<br>3. Essential for A-level Economics paper 1 form five by Ambrose Odhiambo | |

iv. Scientific calculator
v. Godoro futi mbili na nusu kwa sita lenye foronya ngumu
vi. Mashuka rangi ya bluu jozi mbili, blanketi 1, chandarua kimoja cha rangi ya bluu
vii. Nguo za ndani, ndala na kitana
viii. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli, kijiko na kikombe) vyombo vya plastiki haviruhusiwi
ix. Ndoo mbili ndogo ( lita kumi) zenye mifuniko mpya
x. Buti kwa ajiri ya kujikinga kipindi cha mvua
xi. Kwanja 1, jembe lenye mpini 1, panga 1, mifagio 2 wa ndani na wan je(chelewa),sequzer 1
xii. Dawa ya kusafishia choo/tiles. Lita moja
xiii. Tochi kwa ajiri ya dharula

**2.3 Michango mbalimbali**

a) Michango hii ilipwe kwenye AKOUNTI ya shule NMB 22101200129. NGERENGERE SECONDARY SCHOOL.

| Na | Aina ya michango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |

NB: Kumbuka kuleta Risti halisi (pay slip)

b) **Michango hii utakuja kulipia shuleni**

| Na | Aina ya michango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Nembo | 5,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | kitambulisho | 5000/= |
| jumla | | 15,000/= |

**3. Sheria na kanuni mhimu za shule**

Shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria za Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria za Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na kanuni za shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanya kazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani nan je ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

**MUHIMU**:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
- Mwanafunzi awapo shuleni atataakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa shule (Msiba au ugonjwa)

3.2 **Makosa yatakayosababisha mwanfunzi kufukuzwa shule ni pamoja na**;

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kufuga nywele au kufuga ndevu
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
viii. Uvutaji sigara
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa n.k
x. Kusababisha mimba
xi. Kushiriki matendo ya uharifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xiv. Kudharau bendera ya taifa
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatanisho na fomu muhimu**

i. Fomu ya uchunguzi wa Afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya serikali
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
iii. Picha za wazazi au walezi wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu
iv. Kopi ya matokeo ya kidato cha nne(Result slip)
v. Nakala ya cheti cha kuzaliwa

**5. Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya mkuu wa Shule…………………………………

Jina la Mkuu wa Shule: **PETRO HOWARD TUMAI**

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kuwa ni walimu. **UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO**

- Mkuu wa shule 0715106414/0787106414
- Makamu mkuu wa shule 0677724954/0759357458
- Mwandamizi malezi 0753946686/0655946685
- Mwalimu wa malezi msaidizi 0786860443

MEDICAL CERTIFICATE FORM

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF ………………………………… FORM ……….**

Please examine the above named as to his fitness for admission to school as a student.

***Name and signature of requesting Officer.***

Name…………………………………………….. Signature …………..
Date ……………………….
To be completed by a Government Medical Officer in respect of FORM 1/5 entrants:
Pupil's Full Name……………………………………………………………………………………
Blood count (Red and White)
…………………………………………………………………………………………………………….
Stool Examination
……………………………………………………………………………………………………………………….
Urinalysis………………………………………………………………………………………………………………
Syphilis
Test………………………………………………………………………………………………………………………
T. B.
Test………………………………………………………………………………………………………………………
Eye
Test………………………………………………………………………………………………………………………
Ears………………………………………………………………………………………………………………………
Chest……………………………………………………………………………………………………………………
Spleen……………………………………………………………………………………………………………………
Abdomen………………………………………………………………………………………………………………
Blood
Group……………………………………………………………………………………………………………………
ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairments infections, chronic or family diseases etc.
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
I have examined the above named and I consider that he is physically fit/unfit to pursue as stated above.
Name and signature of Certifying Officer.
Name ………………………………………. Signature…………………………………….
Station ……………………………………… Designation ………………………………..
Date ……………………………………… STAMP ……………………………………

## F: FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina ………………………………………………………………. DINI ……………………
2. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………
3. Wilaya ulimozaliwa…………………………………mkoa ………………….
4. Namba ya cheti cha kuzaliwa ……………………………………………….
5. Jina la baba ……………………………………………………………..
6. Kazi ya baba ……………………………………………………………….
7. Anwani ya baba ……………………. Namba ya simu ……………………….
8. Jina la mama ……………………………………………………………….
9. Kazi ya mama ……………………………………………………………..….
10. Anwani ya mama ……………………….. Namba ya simu …………………
11. Shule uliyosoma madarasa madaraka uliyoshika
    ……………………….. ……………………. …………………………
    ………………………... ……………………… ………………………....
12. Je, baba yu hai………………………………………(ndiyo/hapana)
13. Je, mama yu hai……………………………………(ndiyo/hapana)
14. Je, unakaa na mlezi……………………………….(ndiyo/hapana)
15. Anwani ya mlezi ……………………….. namba ya simu ………………………
16. Kazi ya mlezi ……………………………………………………………………..
17. Afya ya mwanafunzi (kama anaugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe. Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha daktari)
    ……………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………
18. WAZAZI/WALEZI NA NDUGU WA MWANAFUNZI NA PICHA ZAO ZIWEKWE HAPO CHINI

**( HAWA TU NDIO WATAKAOTAMBULIKA NA UONGOZI WA SHULE)**

| S/N | JINA | SIMU | UHUSIANO | ANAPOISHI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |

Sahihi ya wanafunzi…………………………………………..Tarehe………………….

Sahihi ya mzazi/mlezi …………………………………………Tarehe……………………….